

Government works on 15-year grand plan to boost protection of fisheries resources

By Guardian Correspondent,

Singida

THE Food and Agriculture Organisation (FAO) of United Nations has issued US\$195,000 (450m/-) to facilitate review and preparation of a 15-year mega-plan aimed at boosting protection of fisheries resources in the country.

Permanent Secretary in the ministry of Livestock and Fisheries Dr Rashid Tamatamah revealed this here yesterday during the three-day stakeholders meeting which aimed to discuss and agree on various priorities which should be incorporated in the plan.

Dr Tamatamah said that the government's zeal is to supervise and ensure that the fisheries sector contributes heavily to the country's income.

"To implement the plan which will be launched next year, we aim to strengthen efforts to ensure that fisheries resources are well protected and governed to bring long-lasting positive impacts to both the government and Tanzanians," he said, adding: "It is our hope that the plan will stimulate economic growth while also improving lives from household level to the national level."

He acknowledged that despite strides to modernize it, the fisheries sector still faces a number of challenges which also calls for coordinated efforts to fight them as they affect the sector's sustainable development.

"To address the challenges, the ministry

has been implementing several measures and initiatives including the forthcoming grand plan scheduled to commence next year," he said.

FAO's fisheries coordinator, Dr Oliver Mkumbo said the organization decided to fund the plan as part of its global plans aimed to eradicate hunger and food insecurity by 2030.

Head of fishermen from Kigoma Region Francis John commended the government for coming up with the plan among its priorities is to support small-scale fishermen and traders to improve their activities.

"Fishers in Lake Tanganyika are so happy to hear the government's supportive programmes that are going to improve their businesses, with the forthcoming improvements; the traders will be able to export their fish products in the global market including the United States, Australia, Canada, United Kingdom (UK) and Denmark.

Raphael John, one of the stakeholders said that the plan will facilitate improvement in the production of marine products including fish (aquaculture), a move which will contribute immensely to reduce dependence from abroad.

"In many developed countries, aquaculture has been given special priority, so it better now, we also invest in the area so that we do not rely solely on freshwater fish, we must start now before the natural resources in seas, rivers and lakes extinct."

Serikali yajipanga kuimarisha sekta ya uvuvi nchini

JAMVI, LA HADJAZI

NA Mwandishi Wetu, Singida

SERIKALI kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ipo katika mchakato wa kukamilisha Mpango kabambe wa miaka 15 ijayo kuanzia 2021 utakaosimamia sekta ya Uvuvi na kutoa dira ya kulinda rasilimali za uvuvi ili sekta hiyo iweze kutoa mchango mkubwa na endelevu katika pato la taifa.

Hilo limeelezwa wakati Kaitibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dk. Rashid Tamatamah akifungua Mkutano wa Wadau wa Sekta ya Uvuvi wa kupitia, kujadili na kuidhinisha masuala ya kipaumbele yanayopaswa kuingizwa katika Mpango huo Kabambe unaofanyika mkoani Singida tangu juzi.

Aidha, Dk. Tamatamah alisema lengo la Serikali ni kuona sekta ya Uvuvi inaendelea kutoa mchango mkubwa katika pato la taifa zaidi ya ilivyosasa na ndio maana inaanda Mpango huo ili usimamizi wa rasilimali za uvuvi uwe imara.

"Ni mategemeo yetu kuwa mpango huu utatoa hamasa kwa sekta ya uvuvi katika kulinda us-

alama wa chakula kuanzia ngazi ya kaya na taifa, vilevile tunatarajia utuingize katika uchumi wa viwanda na uchumi wa bluu," alisema Dk. Tamatamah.

Alisema, pamoja na juhudu za Wizara za kusimamia maendeleo ya Sekta ya Uvuvi nchini, Sekta hiyo imeendele kukabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo kwa ujumla zimekuwa zikiathiri ukuaji na uendelevu wa sekta hiyo.

Aliendelea kueleza kuwa ili kukabiliana na changamoto hizo, Wizara imekuwa ikitekeleza mipango, mikakati na programu mbalimbali zinazolenga kuendeleza sekta ya uvuvi nchini, miongoni mwa mipango hiyo ni Mpango huo Kabambe wa Uvuvi unaotarajiwa kuanza kutumika mwaka 2021.

Mratibu wa Masuala ya Uvuvi kutoka Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO), ambao wana nafadhili maandalizi ya mpango huo, Dk. Oliver Mkumbo alisema shirika hilo limeamua kufadhili mpango huo ikiwa ni sehemu ya malengo yao ya kuhakikisha dunia inaondokana na njaa, umasikini na kuimarisha usalama wa chakula ili ifikapo mwaka 2030 pasiwepo na mtu atakayekuwa na njaa.

Aidha, wadau wa Sekta ya Uvuvi hawakusita kuonesha matumaini yao na mpango huo huku wakisema kuwa ukikamilika utajibu changamoto nyingi ambazo zimeendelea kukabili sekta hiyo.

Kiongozi wa Wavuvi Mkoani Kigoma, Francis John alisema kuwa mpango huo ambao utasimamia rasilimali za uvuvi utawasaidia kuimarisha biashara yao ya dagaa kutoka ziwa Tanganyika kwani mpango huo utawahakikishia uwepo wa dagaa wengi ambapo wataweza kuwa na mzigo wa uhakika wa kusafirisha kwenda kuuza dagaa wao katika nchi za Marekani, Australia, Kanada, Uingereza na Denmark.

Naye, Raphael John, mdau wa sekta hiyo ya Uvuvi alisema kuwa moja ya mambo yatayokwenda kuimarishwa kupitia mpango huo ni ufugaji na ukuzaji wa viumbe maji jambo ambalo anasema litaaidia kupunguza utegemezi wa kupata mazao ya uvuvi kutoka maji ya asili pekee.

"Katika nchi nyingi zilizoendelea, ufugaji na ukuzaji wa viumbe maji umepewa kipaumbele sana, ni muhimu kuimarisha eneo hilo ili tusitegeme tu uvuvi wa mazao ya

samaki katika maji ya asili, ni lazima tuanze sasa kabla rasilimali za asili katika bahari, mito na maziwa hazijaisha," alisema John.

Mpaka sasa sekta ya uvuvi inachangia asilimia 1.7 katika pato la Taifa huku ikielezwa kuwa sekta hiyo inatoa ajira ya moja kwa moja kwa wananchi takriban 202,000 na wananchi wengine wasiopungua Milioni 4.5 wamaendelea kutegemea kupata kipato chao kupitia sekta hiyo.



Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) limetoa Dola za Kimarekani 195,000 kwa ajili ya kufanya mapitio na kuandaa Mpango huo Kabambe wa sekta ya uvuvi ili sekta hiyo iweze kusimamiwa vizuri na kuendelea kuleta maendeleo yenye tija nchini.

Uandaaji wa mpango huo ni sehemu ya mipango mingi ambayo serikali imekusudia kuitekeleza, wakati akifungua Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Novemba 13, 2020 jijini Dodoma, Rais Dk. John Magufuli alieleza mipango kadhaa ya kuboresha sekta ya uvuvi ikiwemo ununuzi wa meli nane, ujenzi wa Bandari kubwa ya uvuvi itakayotoa ajira 30,000.



The Guardian

www.ippmedia.com



LIKE & FOLLOW US

ISSN 0856 - 5434 ISSUE No. 8072• PRICE: Tsh 1,000, Kenya sh100

TANZANIA

SATURDAY 28 NOVEMBER, 2020

RESOURCES



GRAND PLAN TO BOOST FISHERIES RESOURCES' PROTECTION PAGE 3

POLITICS



UNICEF CONGRATULATES DR HUSSEIN ALI MWINYI PAGE 4

WELFARE



SOLUTIONS TO CHALLENGE OF 'STREET CHILDREN' IN TANZANIA PAGE 5

TRANSPORT



NEW MBEZI-LUIS MODERN BUS TERMINAL STARTS TRIAL OPERATIONS PAGE 6

Serikali yajipanga kuimarisha sekta ya uvuvi nchini

NA MBARAKA
KAMBONA, SINGIDA

SERIKALI kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ipo katika mchakato wa kukamilisha Mpango wa miaka 15 ijayo kuanzia 2021 utakao-simamia sekta ya Uvuvi na kutoa dira ya kulinda rasilimali za uvuvi ili sekta hiyo iweze kutoa mchango mkubwa na endelevu katika pato la taifa.

Hilo limefahamika wakati Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dkt. Rashid Tamatamah aki-fungua Mkutano wa Wadau wa Sekta ya Uvuvi wa kupitia, kujadili na kuidhinisha masuala ya kipaumbele yanayopaswa kuingizwa katika Mpango huo Kabambe unaofanyika Mkoani Singida na ulianza Novemba 26 na unatarajia kumalizika leo, 2020.

Dkt. Tamatamah alisema kuwa lengo la Serikali ni kuona sekta ya Uvuvi inaendelea kutoa mchango mkubwa katika pato la taifa zaidi ya ilivyosasa na ndio maana inaanda Mpango huo ili usimamizi wa rasilimali za uvuvi uwe imara.

"Ni mategemeo yetu kuwa mpango huu utatoa hamasa kwa sekta ya uvuvi katika kulinda usalama wa chakula kuanzia ngazi ya kaya na taifa, vilevile tunatarajia utuingize katika uchumi wa viwanda na uchumi wa biu," alisema Dkt. Tamatamah.

Alisema kuwa pamoja na juhudi za Wizara za kusimamia maendeleo ya Sekta

ya Uvuvi nchini, Sekta hiyo imeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo kwa ujumla zimekuwa zikiathiri ukuaji na uendelevu wa sekta hiyo.

Aliendelea kueleza kuwa ili kukabiliana na changamoto hizo, Wizara imekuwa ikitekeleza mipango, mikakati na programu mbalimbali zinazolenga kuendeleza sekta ya uvuvi nchini, miongoni mwa mipango hiyo ni Mpango huo Kabambe wa Uvuvi unaotarajiwa kuanza kutumika mwaka 2021.

Mratibu wa Masuala ya Uvuvi kutoka Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO), ambao wanafadhili maandalizi ya mpango huo, Dkt. Oliver Mkumbo alisema shirika hilo limeamua kufadhili mpango huo ikiwa ni sehemu ya malengo yao ya kuhakikisha dunia inaondokana na njaa, umasikini na kuimarisha usalama wa chakula ili ifikapo mwaka 2030 pasiwepe na mtu atakayekuwa na njaa.

Aidha, wadau wa Sekta ya Uvuvi hawakusita kuonesha matumaini yao na mpango huo huku wakisema kuwa ukikamilika utajibu changamoto nyingi ambazo zimeendelea kukabilika sekta hiyo.

Kiongozi wa Wavuvi Mkoani Kigoma, Francis John alisema kuwa mpango huo ambao utasimamia rasilimali za uvuvi utawasaidia kuimarisha biashara yao ya daga kutoka ziwa Tanganyika kwani mpango huo utawahakikisha uwepe wa daga wengi ambapo



wataweza kuwa na mzigo wa uhakika wa kusafirisha kwenda kuuza daga wao katika nchi za Marekani, Australia, Kanada, Uingereza na Denmark.

Naye, Raphael John, mdau wa sekta hiyo ya Uvuvi alisema kuwa moja ya mambo yatayokwenda kuimarishwa kupitia mpango huo ni ufugaji na ukuzaji wa viumbe maji jambo ambalo anasema litasaidia kupunguza utegemezi wa kupata mazao ya uvuvi kutoka maji ya asili pekee.

"Katika nchi nyingi zilizoendelea, ufugaji na ukuzaji wa viumbe maji umepelewa kipaumbele sana, ni muhimu kuimarisha oneo

hilo ili tusitegeme tu uvuvi wa mazao ya samaki katika maji ya asili, ni lazima tuanze sasa kabla rasilimali za asili katika bahari, mito na maziwa hazijaisha," alisema John.

Mpaka sasa sekta ya uvuvi inachangia asilimia 1.7 katika pato la Taifa huku ikielezwa kuwa sekta hiyo inatoa ajira ya moja kwa moja kwa wananchi takriban 202,000 na wananchi wengine wasiopungua Milioni 4.5 wamaendelea kutegemea kupata kipato chao kupitia sekta hiyo.

Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) limetoa Dola za Kimarekani 195,000 kwa ajili ya kufanya mapitio

na kuandaa Mpango huo Kabambe wa sekta ya uvuvi ili sekta hiyo iweze kusimamiwa vizuri na kuendelea kuleta maendeleo yenye tija nchini.

Uandaaji wa mpango huo ni sehemu ya mipango mingi ambayo serikali imekusudia kutekeleza, wakati akiifungua Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Novemba 13, 2020 jijini Dodoma, Mhe. Rais, Dkt. John Joseph Magufuli alieleza mipango kadhaa ya kuboresha sekta ya uvuvi ikiwemo ununuzi wa meli nane (8), ujenzi wa Bandari kubwa ya uvuvi itakayotoa ajira 30,000.